HOTUBA YA MHESHIMIWA BENEDICT NGALAMA OLE NANGOLO (MB), NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA TANO WA BARAZA LA MWAKA LA WADAU WA TASNIA YA NYAMA TANZANIA, TAREHE 28 FEBRUARI 2013 GLONENCY 88 HOTEL, MOROGORO

Mhe. Joel N. Bendera, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,
Dkt. Charles Nyamrunda, Katibu Mkuu, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi,
Dkt. Ben Moshi, Mwenyekiti wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,
Prof. Faustin Lekule, Mwenyekiti wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Ndugu, Wajumbe wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama,
Ndugu, Wajumbe wa Bodi ya Nyama Tanzania,
Ndugu, Wawakilishi wa Wizara na Taasisi za Serikali,
Ndugu, Wawakilishi wa Taasisi zisizo za Kiserikali (NGO),
Wageni Waalikwa,
Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mwenyekiti, Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru waandaaji kwa kunipa fursa hii ya kufungua mkutano wa tano wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama. Najisikia kupewa heshima kubwa ya kuwa mmoja wa washiriki wa mkutano huu. Pia, napenda kutoa pongezi zangu maalumu kwa wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuteuliwa kuwa wawakilishi wa wadau katika Baraza hili muhimu kwa maendeleo ya tasnia ya Nyama nchini, hii ni kwa sababu nilikuwa sijapata nafasi ya kuwapongeza. Naamini uteuzi wenu umetokana na sifa na uwezo wa kiutendaji mliouonyesha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi zilizowapendekeza.

Aidha,Najisikia kuwiwa kuzipongeza Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanikisha kuleta wajumbe kushiriki katika mkutano wa kisheria wa Baraza la Mwaka la Wadau wa Tasnia ya Nyama. Hii inadhihirisha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa, nanyi wajumbe mmeelewa kuwa jukumu la kuendeleza tasnia ya nyama hapa nchini ni la wadau wote. Hivyo, ninatoa mwito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo hazikuwakilishwa kwenye Baraza hili, kuiga mfano huu na kutekeleza jukumu hili la kisheria.

Mwisho kwa kutaja, napenda kuwashukuru wenyeji wetu wa mkoa wa Morogoro kwa kukubali kuwa wenyeji kwa mara nyingine na kwa mapokezi mazuri ya wadau waliohudhuria katika mkutano huu.

Ndugu Mwenyekiti; nimeambiwa kwamba mtakuwepo hapa kwa siku mbili tu, naamini mtazitumia vizuri siku hizi kadri itakavyowezekana kujadili maudhui ya mkutano ambayo ni

mafanikio, changamoto, fursa na mikakati ya kuendeleza biashara ya nyama kiushindani, ili kuiwezesha Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazozalisha nyama kwa ubora na wingi. Ninafahamu kwamba miongoni mwa majukumu ya Baraza hili ni kusimamia maendeleo ya tasnia ya nyama na utekelezaji wa Sheria zinazoongoza tasnia ya nyama kwa ujumla ikiwa ni pamoja na Sheria ya:-

a. Usalama wa Chakula, Madawa na Vipondozi Na 1 ya Mwaka 2003;
b. Magonjwa ya Mifugo Na. 17 ya Mwaka 2003;
c. Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006;
d. Biashara ya Ngozi Na 18 ya Mwaka 2008;
e. Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya Mwaka 2008;
f. Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo na Mazao yake Na.12 ya Mwaka 2010; na
g. Nyanda za Malisho na Vyakula vya Mifugo Na. 13 ya Mwaka 2010.

Pamoja na majukumu hayo, Baraza hili linafanya kazi kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Malengo ya Kimataifa ya Millenia (MDGs) na Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Pia kuzingatia Sera ya Mifugo ya mwaka 2006, mkakati wa kutekeleza sera hiyo, mpango wa Taifa wa maendeleo wa miaka mitano (2011/12 -2015/16), mipango ya kuendeleza sekta ya KILIMO KWANZA, Mpango wa Uwekezaji katika Kilimo na Uhakika wa Chakula (Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan – TAFSIP), Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania (SAGCOT) pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2010. Ni miaka **mitano** sasa tangu Baraza hili lizinduliwe na mmekuwa mkijadili na kutathimini namna bora ya kuendeleza tasnia na kujipanga kuzalisha nyama yenye ubora. Ni vema Baraza hili likajipima kwa kipindi hiki limefanikiwa kiasi gani kukuza biashara ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, napenda sasa kuongelea uwezo wa Tanzania katika kuzalisha na biashara ya nyama. Ninajivunia kwamba Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali kubwa ya eneo la malisho na mifugo. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania ina ukubwa wa hekta milioni 88.6 za ardhi na kati ya hizo, hekta milioni 60 ni za malisho, zinazoweza kulisha mifugo takriban ng'ombe wakubwa milioni ishirini. Vile vile ina takribani Ng'ombe milioni 18.8, Mbuzi milioni 13.1, Kondoo milioni 3.6, Nguruwe milioni 1.37, Kuku wa kienyeji milioni 33 na wa kisasa milioni 20. Sehemu kubwa ya mifugo hii ni ya asili na inatumika kuzalisha nyama ikilinganishwa na ng'ombe wa maziwa 605,000, kuku milioni 8 wa mayai ambao pia huzalisha nyama baada ya mzunguko wa uzalishaji wa mazao haya.

Kutokana na takwimu hizi, ni dhahiri kwamba Tanzania ina fursa kubwa ya kuendeleza zao la nyama kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Takwimu za biashara ya mifugo na nyama zinaonyesha kwamba idadi ya ng'ombe waliouzwa kwenye minada yetu inaongezeka kutoka ng'ombe 779,260, mbuzi 616,693 na kondoo 112,995 katika mwaka 2007/2008 hadi kufikia ng'ombe 781,230, mbuzi 623,732 na kondoo 114,564 katika mwaka 2011/2012. vivyo hivyo uzalishaji wa nyama umeongezeka toka tani 410,706 mwaka 2007/08 hadi tani 422,230 mwaka 2011/12, hata hivyo ongezeko hili halikuonyesha badiliko kubwa la ulaji wa

nyama yaani kilo 11 hadi kilo 12 kwa mtu kwa mwaka sawia ikilinganishwa na kilo 50 zinazopendekezwa na FAO.

Aidha, kumekuwa na ongezeko la mauzo ya nyama nje ya nchi kutoka tani 10.7 za nyama ya ng'ombe na tani 98.6 za nyama ya mbuzi na kondoo kwenda nchi za Falme za Kiarabu, Kuwait na Oman katika mwaka 2007, hadi kufikia tani 139.8 za nyama ya ng'ombe, tani 35.4 za nyama ya kondoo na tani 46.7 za nyama ya mbuzi kwenda nchi za Kuwait, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Misri na Oman katika mwaka 2011/12, takwimu hizi zimeonyesha ipo fursa kwa nchi yetu kufanya biashara hii ingawa juhudi zaidi zinahitajika. Tanzania imeuza ng'ombe 2,970, mbuzi na kondoo 302 kwenda nchi za Comoro, Kenya na Burundi. imeweza kuuza ng'ombe 3,264, mbuzi na kondoo 1,834 kwenda nchi za Comoro, Kenya, Burundi na Malawi.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba wajumbe wa Baraza lako wanawakilisha wadau wote wa tasnia ya nyama, ni dhahiri kwamba sehemu kubwa ya wanaowakilishwa ni wafugaji wa asili ambao ni takribani kaya milioni 1.8 wanamiliki rasilimali kubwa ya mifugo zaidi ya asilimia 90.
Aidha, uvunaji wa mifugo mashambani ni kati ya asilimia 4 na 5 kwa mwaka, badala ya kiwango kinachotakiwa cha asilimia 15 – 30 kwa mwaka. Hii inasababishwa na kutovuna mifugo kwa wakati na kutozingatia ubora wa mifugo inayohitajika katika soko. Hatuna budi kuelimishana na kutambua umuhimu wa kuvuna mifugo, hali ambayo itatusaidia kuuza mifugo mingi yenye ubora na bei nzuri kwa mwaka.

Changamoto

Ndugu Mwenyekiti, kwa kuwa sisi ni wadau wa sekta ndogo ya nyama, ingekuwa vema tukaitazama sekta hii kwa umakini zaidi. Takwimu za uzalishaji wa nyama zinaonyesha kuwa kumekuwepo na upungufu katika uzalishaji wa nyama kutoka tani 210,370 katika kipindi cha mwaka 2005/06 ikilinganishwa na tani 180,629 mwaka 2006/07. Sote tunafahamu kwamba upungufu huu ulisababishwa na kuwepo kwa mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa ama RVF. Naamini kwamba mwaka 2007/2008 uzalishaji utapanda maana hali ni swari. Jambo jingine ambalo halifurahishi kuhusu sekta hii ndogo ya nyama ni kwamba kiwango cha ulaji wa nyama

ni wastani wa kilo 10 kwa mtu kwa mwaka, ambacho ni chini ya kiwango cha kimataifa kinachopendekezwa na FAO cha kilo 50 kwa mtu kwa mwaka.

Ndugu Mwenyekiti, inawezekana sababu mojawapo ya kukua kwa kasi ndogo ya uzalishaji wa nyama ni kutokuwepo kwa chombo cha kusimamia uzalishaji wa mifugo, biashara ya mifugo na viwanda vya kusindika nyama. Upungufu huo umeifanya nchi yetu kuwa na uzalishaji mdogo na kukosa soko la uhakika la mifugo. Kumbukumbu zinaonyesha kuwa katika miaka ya hamsini na baada ya uhuru, Tanzania ilikuwa na Kampuni binafsi ya Tanganyika Packers Limited (TPL) iliyokuwa inamiliki kiwanda cha kusindika nyama na kuendesha biashara ya nyama hapa nchini. Mwaka 1974 kiwanda hicho cha TPL kilitaifishwa kutekeleza sera ya wakati ule ya kuuweka uchumi wa nchi mikononi mwa wananchi. Kinyume na matarajio ya kuongeza tija, kiwanda hicho kilishindwa kujiendesha kwa ufanisi hivyo kupoteza cheti cha usafi (UK Sanitary Certificate) na kusitishwa kwa mkataba wa kuuza nyama kwenye kampuni ya Brooke Bond Lieberg Ltd nchini Uingereza. Bila shaka kiwanda kilipoteza sifa kutokana na usimamizi uliolegalega wakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi karibuni biashara ya mifugo imepata msukumo kupitia jitihada mbali mbali za serikali, ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya miundombinu ya masoko hususan ujenzi na ukarabati wa minada ili kuongeza upatikanaji wa mifugo ya nyama kwa lengo la kukidhi soko la ndani na la nje. Vile vile Serikali ilijenga Machinjio ya kisasa na Chuo cha Ukataji Nyama mjini Dodoma kwa nia ya kuongeza thamani ya mifugo na nyama pamoja na kutoa elimu ya uzalishaji wa nyama. Kadhalika mwaka jana tumetoa matangazo ya kukaribisha wawekezaji binafsi kushirikiana na Serikali, kupitia Kampuni yake ya NARCO kujenga viwanda vya nyama na machinjio mapya. Nafurahi kuona kwamba wapo watanzania walioonyesha nia ya kuwekeza na mchakato wa kuanza kazi hiyo unaendelea. Pia naomba kuwapongeza wenzetu ambao tayari wameanzisha viwanda na machinjio binafsi, kwa mfano Kampuni ya SAAFI kule Sumbawanga, Kampuni ya Tanzania Pride Meat kule Morogoro na Kampuni ya Triple S ambao watawekeza kule Shinyanga. Aidha naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza wafanyabiashara ya nyama ambao wameweza kuiweka Tanzania kwenye ramani ya dunia kwa nchi zinazouza na kusafirisha ng'ombe na nyama nje ya nchi. Takwimu zinaonyesha kwamba Tanzania imeweza kuuza ng'ombe 3,818 na mbuzi 606 kwenda nchi za Comoro na Burundi. Aidha, tumeuza kilo 10,701 za nyama ya ng'ombe kwenda nchi za Falme za Kiarabu na Oman na kilo 98,551 za nyama ya

mbuzi na kondoo kwenda Oman, Falme za Kiarabu na Kuwait katika mwaka 2007, takwimu ambazo zinatia moyo kwa kuanzia.

Ndugu Mwenyekiti, katika juhudi za kuwashawishi wafugaji kuvuna mifugo yao, serikali kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imeendelea kuelimisha juu ya mlolongo wa matukio ya uzalishaji wa zao la nyama unaoanzia kwenye uzalishaji wa mifugo. Uzalishaji wa mifugo bora hapa nchini umekuwa changamoto kubwa, kuanzia kwenye ubora wa mifugo yenyewe, mifumo ya uzalishaji, matumizi bora ya ardhi, upatikanaji wa malisho bora, maji ya kutosha na udhibiti wa magonjwa. Vile vile mifugo mingi inayozalishwa hapa nchini ni ya asili yenye umbo dogo na hukuwa kwa kasi ndogo, jambo ambalo linasababisha kuchelewa kuvuna, kuzalisha nyama isiyokidhi viwango vya ubora na uvunaji wa kiasi kidogo cha nyama. Aidha, ufugaji wa ranchi zinazojumuisha ranchi za Taifa na za wawekezaji wa ndani unawakilisha takribani asilimia 2 tu za mifugo yote hapa nchini. Hata hivyo, kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji kwenye ranchi hizi endapo mbinu ya unenepeshaji itatumika. Ufugaji huu utawezesha kununua mifugo kutoka kwa wafugaji wadogo wadogo na kuwanenepesha (finishing) kwenye ranchi hizi kabla ya kuchinja. Kwa kufanya hivyo wafugaji watapata soko la uhakika la mifugo yao, watajifunza na kuhamasika kufuga kibiashara, kuinua kipato chao na kuchangia katika kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kukuza Kipato na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Aidha, mlolongo wa uzalishaji wa zao la nyama hapa nchini hauzingatii kanuni za viwango vya ubora wa mazao zikiwa ni pamoja na kuwa na mfumo wa uendelezaji wa mbegu bora (breeding system), mfumo wa utambuzi, uandikishaji na ufuatiliaji, viwango vya ubora na usafi wa mazao ambavyo vinakidhi mahitaji ya walaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa sasa mfumo mzima wa uongezaji wa thamani wa zao la nyama umedumaa, hata hivyo zipo fursa nyingi katika kuongeza thamani ya zao la nyama ikiwa ni pamoja na kuboresha uhifadhi, kuimarisha usindikaji na kufungasha bidhaa za nyama. Fursa hizi zikiendelezwa kwa utaratibu wa kipaumbele tutaweza kuboresha hali iliyopo sasa.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba vipo viwanda/machinjio takribani saba vyenye uwezo mdogo na wa kati wa kuchinja na kusindika nyama na bidhaa zake kwa siku. Viwanda hivyo ni pamoja na Arusha Meat Company (ng'ombe 150 na mbuzi 200), Tanzania Meat Company (Dodoma Abattoir ng'ombe 150 na mbuzi 200), SAAFI ya Sumbawanga (ng'ombe 225 na mbuzi 400), Tanzania Pride Meat (ng'ombe 150 na kondoo 200, kuku 8000), Interchick (kuku 3,000), usindikaji, TANMEAT 2002 Ltd, Dar es Salaam (kusindika kilo 1000 kwa siku), Happy sausage, Arusha (ng'ombe 80 kwa wiki). Juhudi za kuwekeza kwenye viwanda vya kusindika nyama zinaendelea, juhudi ambazo zimeanza kuonyesha mafanikio ni pamoja na kujenga machinjio ya Ruvu

ambayo itakapo kamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe 800 na mbuzi 400 na Manyara Ranchi (ng'ombe 100 na mbuzi 200). Vile vile serikali imeendelea kuhamasisha wawekezaji kuwekeza/kufufua machinjio ya Tripple S ya Shinyanga na TPL ya Mbeya.

Ndugu Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la viwanda vya kusindika na kuongezea thamani zao la nyama, uwekezaji mdogo unaotokana na uwezo mdogo wa kimitaji, teknolojia duni, ukosefu wa mfumo wa upashanaji habari na ushirikiano kati ya wafanyabiashara wa nyama na walaji imekuwa changamoto kubwa katika maendeleo ya viwanda vya kusindika na kufungasha bidhaa za nyama. Kushindwa kuendeleza ranchi ndogo ndogo zilizogawiwa kwa wawekezaji wa ndani, usindikaji wa chini ya uwezo wa kiwanda katika viwanda vilivyopo, mifano ni SAAFI (50%), Arusha Meat Company (50%), TANMEAT 2002 (10%), Interchick (50%), Tanzania Meat Company (50%). Aidha uzalishaji wa nyama ya kiwango cha chini cha ubora katika machinjio zetu za Halmashauri na kufungwa kwa viwanda vya Tanzania Pride Meat cha Morogoro na Mkuza cha mkoa wa Pwani ni baadhi ya mifano hai ya uwezo mdogo wa kimitaji wa wawekezaji katika sekta ya nyama. Tujiulize tatizo liko wapi? Ni jambo gani linalotukwamisha kuingia katika uzalishaji na usindikaji nyama kibiashara? Je ni upungufu wa elimu na utaalam? Je ni uwezo mdogo wa kimitaji? Je kutokuwa na mifugo ya kutosha? Je ni ufunyu wa soko? Pengine jibu ni kwamba hatujajizatiti kimkakati kuendeleza mlolongo wa zao la nyama? Ni dhahiri kwamba wakati sasa umefika kwa kila mmoja wetu kujiangalia katika nafasi yake na kuona namna ambavyo anaweza kuchangia katika kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa. Ninaamini kuwa leo tutakubaliana sote juu ya namna ambavyo tunapaswa kujipanga katika kuinusuru sekta hii muhimu ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, kwa muda mrefu sasa, sekta ndogo ya nyama imekuwa ikiendeshwa kihohela bila kuwa na taratibu, miongozo na usimamizi, jambo hili limefanya maendeleo ya sekta hii kudumaa. Sote tunafahamu kwamba hali hii ndiyo ilifanya tujitahidi kutung Sheria ya Nyama Na. 10 ya Mwaka 2006, sheria iliyounda Baraza hili lenye wajumbe wanaowakilisha wadau mbalimbali kutoka katika Halmashauri zote za wilaya za Tanzania Bara, vyama vya kitaifa vya wadau (wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara), mashirika yasiyo ya kiserikali, wizara na taasisi mbali mbali za serikali. Baraza lina jukumu la kuhamasisha maendeleo ya sekta ndogo ya nyama pamoja na Bodi ya Nyama Tanzania ikiwa ni msimamizi mkuu wa utekelezaji wa sheria hii. Kwa uwakilishi huu, nina imani kwamba Baraza hili litaweza kujadili hoja muhimu, na kupata michango toka kwa wadau mnaowawakilisha itakayowezesha kuweka mikakati endelevu ya kuiendesha sekta ndogo ya nyama kwa ufanisi.

Ndugu Mwenyekiti, kuundwa kwa vyombo hivi vya usimamizi wa sheria, vinavyofanya kazi kama jukwaa la wadau kwa kutoa ushawishi na uwakilishi kupitia vyama vya

wadau katika ngazi ya Taifa ni sehemu ya juhudi za serikali kujenga mazingira ya kuvutia uwekezaji wa ndani na nje, katika ngazi zote za mlolongo wa kuongeza thamani ya zao la nyama. Ni muhimu kwenu ninyi wadau wa sekta kuangalia namna ambavyo mnaweza kujipanga kwa kuhamasisha uundaji na uimarishaji wa vikundi na vyama vya ushirika wa wafugaji kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, napenda kuwakumbusha wajumbe wa Baraza hili kwamba umoja ulio imara ni ule wenye uwezo wa kifedha, unaofanya mikutano yake kwa mujibu wa katiba, unaohamasisha ushiriki wa wanachama wake katika shughuli mbali mbali za maendeleo na unaoweza kushawishi na kutetea hoja za maendeleo ya sekta katika majukwaa mbali mbali. Ni kwa kushirikiana tu ndipo mtakapoweza kuimarisha mfumo wa kuongeza thamani wa zao la nyama ikiwa ni pamoja na ufugaji mifugo bora, usindikaji wa bidhaa zenye ubora wa hali ya juu unaokidhi mahitaji ya soko la ndani na la nje ili kuwa na biashara inayohimili ushindani na kutoa ushawishi kwa watanzania walio wengi kula nyama bora, safi na salama kwa ajili ya kujenga afya zao na kukuza soko la ndani.

Ndugu Mwenyekiti, pamoja na utajiri huu mkubwa wa raslimali ya mifugo, bado uzalishaji, uvunaji na mauzo ya mazao ya mifugo, hususan maziwa, ngozi na nyama ni duni sana nchini. Sababu za uduni huu ni pamoja na ukosefu wa ardhi, malisho na maji ya kutosha; uhaba wa miundombinu ya masoko; uhaba wa huduma za tiba na udhibiti wa magonjwa; wadau kutokuwa na habari za kutosha juu ya mahitaji ya soko la nyama k.m ladha ya nyama ipendwayo na soko, kiasi sahihi cha mafuta kwenye nyama na kukatwa kwa kiasi na jinsi walaji wanavyotaka. Aidha, ukosefu wa machinjio ya kisasa ya kutosha na viwanda vya kusindika nyama navyo vimechangia kudumaa kwa ufanisi wa sekta ndogo ya nyama nchini. Tatizo sugu la ukame pia limeripotiwa kuchangia sana katika ufanisi mdogo wa sekta ndogo ya nyama.

Pamoja na changamoto hizi, sekta ndogo ya nyama imeendelea kuchangia upatikanaji wa chakula, fedha za kigeni na pato la taifa. Aidha, sekta ndogo ya nyama imewezesha nchi kutotumia akiba ya fedha zake za kigeni kuagiza nyama toka nje. Michango hii inatokana na juhudi za wafugaji wenyewe wadau na serikali kukazana katika kuendeleza sekta hii ndogo ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji endapo mbinu za kuendeleza malisho, kufuga mifugo bora zaidi, kudhibiti magonjwa pamoja kulenga uzalishaji unaozingatia mahitaji ya soko. Serikali itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wenye tija na wa kibiashara ili kuinua kipato cha wafugaji, hivyo

kuchangia katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Pia, napenda kuwapongeza wafugaji wote hususan wafugaji wa asili kwa kuiendeleza sekta ndogo hii licha ya changamoto nilizozitaja hapo juu. Juhudi za wafugaji wa asili zinachangia soko la nyama kwa zaidi ya asili mia 90.

Ndugu mwenyekiti, kuna usemi usemao kuwa *nyama yote ni majani* kwa maana ya kwamba ubora wa nyama hutegemea sana ubora wa malisho. Wingi na ubora wa malisho ndio msingi wa ubora wa nyama, na hivyo Baraza lako halina budi kushauri wadau wa nyama kusaidia kutoa elimu kwa wafugaji juu kuendeleza malisho. Malisho yaliyoko ni ya asili na wingi na ubora wake hupungua kulingana na msimu wakati mbinu za uzalishaji, uvunaji na hifadhi hazijaboreshwa na uwekezaji katika eneo hili ni mdogo.

Napenda kutoa wito kwa Halmashauri za wilaya hususan zile zilizoko katika kanda zenye mifugo, kuhimiza maendeleo ya malisho kwa lengo la kuboresha lishe ya mifugo na hatimaye kuongeza ubora wa nyama. Wizara yangu itaendelea kuhakikisha mbegu bora za malisho pamoja na mbegu bora ya mifugo wa nyama zinapatikana ile kuendeleza sekta ya mifugo kwa ujumla na kipekee kuendeleza sekta ndogo ya nyama.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba vipo viwanda/machinjio takribani saba vidogo na vya kati vya kuchinja na kusindika nyama na bidhaa zake. Viwanda hivyo ni pamoja na *Arusha Meat Company* (ng'ombe 150 na mbuzi 200), *Tanzania Meat Company* - Dodoma (ng'ombe **200** na mbuzi **200**), SAAFI - Sumbawanga (ng'ombe **225** na mbuzi **400**), *Tanzania Pride Meat* (ng'ombe **150** na kondoo **200**, kuku **8,000**), Interchick (kuku **3,000**), Mkuza; TANMEAT 2002 Ltd, Dar es Salaam (kinasindika **tani 1** kwa siku), Happy Sausage - Arusha (ng'ombe **80** kwa wiki). Juhudi za Serikali na sekta binafsi kuwekeza kwenye machinjio/viwanda vya kusindika nyama zinaendelea ambapo unahusisha ujenzi wa machinjio ya Ruvu ambayo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **800** na mbuzi **400** kwa siku na machinjio ya Manyara Ranchi itakayokuwa na uwezo wa kuchinja ng'ombe **100** na mbuzi **200** kwa siku.

Ndugu Mwenyekiti, ninafahamu kwamba pamoja na ongezeko la viwanda vya kusindika na kuongeza thamani zao la nyama, uwekezaji mdogo unaotokana na uwezo mdogo kimitaji, teknolojia duni, mfumo hafifu wa upashanaji habari na ushirikiano kati ya wadau mbalimbali imekuwa changamoto kubwa kwa maendeleo ya viwanda vya kusindika na kufungasha nyama. Kushindwa kuendeleza ranchi ndogo ndogo zilizogawiwa kwa wawekezaji wa ndani na usindikaji wa chini ya uwezo wa kiwanda katika viwanda vilivyopo ambapo mifano ni SAAFI **(50%)**, Arusha Meat Company **(50%)**, TANMEAT 2002 **(10%)**, Interchick (50%), Tanzania Meat Company **(50%)**. Aidha, uzalishaji wa nyama kwa kiwango cha chini cha ubora katika machinjio za Halmashauri na kufungwa kwa viwanda vya Tanzania Pride Meat cha Morogoro ni baadhi tu ya changamoto zilizopo. Jambo hili linakwamisha maendeleo ya usindikaji na uongezaji wa thamani wa zao la nyama, Ni vema tukajiuliza kuwa hali hii itaendelea mpaka lini? Wakati sasa umefika kwa kila mmoja wetu kujiangalia katika nafasi yake na kuona namna atakavyoweza anaweza kuchangia katika kuongeza mchango wa sekta katika pato la Taifa. Ninaamini kwamba mkutano huu wa tatu wa ngazi ya juu ya maamuzi utaliangalia suala hili kwa undani na kuweka mkakati wa kuinusuru sekta hii muhimu.

Ndugu Mwenyekiti, Baraza lako pamoja na Bodi ni vyombo vilivyoundwa kisheria ili viwe jukwaa la wadau katika kutetea maslahi muhimu ya wadau na masuala yanayojitokeza katika uendelezaji wa sekta na kushawishi mabadiliko katika nyanja mbali mbali za kiutendaji. Sheria ya Nyama Na 10 ya Mwaka 2006 inahimiza kuwepo wa vyama vya wadau vyenye nguvu katika ngazi ya Taifa kama sehemu ya juhudi za serikali kujenga mazingira ya kuwezesha wadau kushirikiana na serikali katika kuleta maendeleo ya sekta kwa kuwezesha kuwepo kwa *Public Private Dialog*. Kutokana na umuhimu wa vyama vya wadau serikali imaainisha suala hili katika Ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama nilivyoanisha hapo juu. Nimeelezwa kwamba katika baraza hili wapo wawakilishi wa vyama ambavyo sio hai. Napenda kuwakumbusha wadau wa sekta hii kwamba vyama vilivyo imara ni vile vyenye uwezo wa kifedha, vinavyofanya mikutano yake kwa mujibu wa katiba, vinavyohamasisha ushiriki wa wanachama wake katika shughuli mbali mbali za maendeleo na vinavyoweza kushawishi na kutetea hoja za maendeleo ya sekta katika majukwaa mbali mbali.

Hivyo basi, naagiza kwamba vyama hivyo vifufuliwe na kuimarishwa kwa kujengewa uwezo ili viweze kutekeleza majukumu yake. Ni kwa kushirikiana tu ndipo tutaweza kuweka na kuimarisha mfumo wa uzalishaji na kuongezea thamani zao la nyama kwa kuweka mawasiliano ya kibiashara kati ya wafugaji, wafanyabiashara, wasindikaji na walaji mawasiliano yatakayowezesha wadau kupeana mrejesho chanya katika jitihada za kuzalisha mifugo bora, nyama na bidhaa za nyama zenye ubora unaokidhi mahitaji ya soko na kumfikia mlaji kwa wakati. Kufanya hivyo tutawezesha kuwa na biashara inayohimili ushindani na kutoa ushawishi kwa watanzania walio wengi kula nyama bora, safi na salama kwa lengo la kujenga afya zao na kukuza soko la ndani la nyama.

Katika kuendeleza na kukuza nyama nchini, sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006, inatoa maelekezo kwamba: (1) uendelezaji wa koo bora za ng'ombe kwa ajili ya nyama; (2) uboreshaji wa koosaafu kwenye ng'ombe wa asili; (3) Serikali kuwezesha na kuimarisha utoaji wa huduma za kitaalam; (4) kuhamasisha juu ya uanzishwaji wa vyama vya kifugaji; (5) kuanzisha mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo na mazao yake.

Ndugu Mwenyekiti, pamoja na utajiri mkubwa wa raslimali ya mifugo iliyopo, bado sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto za uzalishaji, uvunaji na mauzo ya mazao ya mifugo hususan maziwa, ngozi na nyama zinazosababishwa na kosaafu za mifugo ya asili; ukosefu wa ardhi na malisho ya kutosha; ukame wa mara kwa mara; uhaba wa miundombinu ya masoko; uhaba wa huduma za tiba na udhibiti wa magonjwa; wadau kutokuwa na habari za kutosha juu ya mahitaji ya soko la nyama. Aidha, utumiaji wa chini wa uwezo wa machinjio za kisasa na viwanda vya kusindika nyama zimechangia kudumaa kwa ufanisi wa tasnia ya nyama nchini.

Pamoja na changamoto hizi, tasnia ya nyama imeendelea kuchangia upatikanaji wa chakula, pato la taifa, fedha za kigeni na kuiwezesha nchi kutotumia akiba ya fedha zake za kigeni kuagiza nyama kutoka nje. Michango hii inatokana na juhudi za wafugaji wote hususan wafugaji wa asili, wadau wengine na Serikali katika kuendeleza tasnia ya nyama. Napenda kutoa wito kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa hususan zile zilizoko katika kanda zenye mifugo mingi, pamoja na kuendelea kutatua changamoto nyingine ziangalie kwa jicho la pekee utengaji, upimaji na umilikishaji wa maeneo ya malisho na ufugaji na kuhakikisha yanatumika vema ili kupunguza migogoro ya ardhi. Halmashauri ziendelee kutoa kiupaumbele kwa shughuli za ufugaji katika kuleta maendeleo na ziweke taratibu nzuri za kuwahamasisha wafugaji kufuga kibiashara na kuvuna kwa wakati.

Ndugu Mwenyekiti, kulingana na takwimu zilizopo zinaonyesha nchi yetu ilikuwa inakumbwa na hali ya ukame karibu kila baada ya miaka kumi. Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, kwa sasa nchi yetu inakumbwa na ukame baada ya kipindi kifupi. Mathalani, katika kipindi cha miaka minne kati ya mwaka 2006 - 2009, nchi yetu ilikumbwa na ukame mwaka 2006 na mwaka 2009. Mabadiliko ya tabianchi siyo tu yameathiri mifumo ya wafugaji wa asili bali yamesababisha kupoteza mifugo mingi na kuathiri maendeleo ya tasnia ya nyama nchini. Ili kupunguza madhara ya mabadiliko haya, Baraza halina budi kushirikiana na asasi za kijamii na kuandaa mikakati itakayowasaidia wafugaji kukabiliana na hali hii.

Ndugu Mwenyekiti, tutakubaliana kwamba bado kuna fursa kubwa ya kuongeza uzalishaji endapo mbinu za kuendeleza malisho, kufuga mifugo bora zaidi, kudhibiti magonjwa pamoja kulenga uzalishaji unaozingatia mahitaji ya soko itazingatiwa. Serikali itaendelea kuhamasisha wadau kuwekeza katika ufugaji wenye tija na wa kibiashara ili kuinua kipato cha wafugaji, hivyo kuchangia katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA).

Soko huria – kutokuwa na vikwazo vya kibiashara

- Kuzingatia ubora na usalama wa mifugo, nyama na bidhaa za nyama ili kuhimili ushindani
- Kuwa na mfumo wa utambuzi na ufuatiliaji wa mifugo, nyama na bidhaa zake ili kumhakikishia mlaji ubora na usalama wa bidhaa
- Kuongeza thamani mifugo, nyama na bidhaa zake

Madhara: - uingizaji mkubwa wa nyama na bidhaa zake (takwimu trend kwa miaka 3, kwa mwezi mwaka huu)

- Kudumaa kwa maendeleo ya tasnia
- Kukosa soko la uhakika la nyama na bidhaa zake

Fursa: masoko ya migodini, hoteli za kitalii na supermarket

Vyama vya wadau au ushirika wa wadau

- Kuanzishwa kwa chama cha kikanda ambapo Tanzania ni mwanachama (NEALCO)
- Kuimarisha vyama vya wadau ndani ili kunufaika na fursa za masoko kikanda
- Kuanzisha majukwaa ya wadau wa tasnia ya nyama katika mikoa na kuimarisha (Mbeya, Iringa, Rukwa na Mwanza) yaliyoanzishwa kwa usimamizi wa SNV ili kutoa fursa ya kuwasiliana na wadau wengine kuhusu namna bora ya kuendeleza tasnia
- Kushiriki katika mkutano wa Baraza kila mwaka kama jukwaa la wadau wa tasnia ya nyama ambapo wadau hupata fursa ya kuwasiliana

Kutambua wadau/ kusajili (SAGCOT IDEA)

- Kutambua wadau wa tasnia ya nyama (nani anafanya nini na yuko wapi)
- Kutambua mahitaji ya kibiashara (nini kinahitaji ili kufanya vizuri zaidi)
- Kutambua namna bora ya kushirikiana ili kupanua wigo wa manufaa kwa wadau wengi zaidi (wengine wananufaaikaje)

Faida zake

- kuimarisha mawasiliano ya kibiashara
- kuwa na uwezo wa kuzalisha kwa kiasi, ubora na kwa wakati na kukidhi mahitaji ya soko hivyo kuwa na soko la uhakika la ndani na kupenya kwenye soko la kikanda na kimataifa

Uwekezaji mkubwa kwenye tasnia

- kuendeleza vitalu kwa kuboresha malisho, miundombinu na koosaafu za mifugo iliyopo
- Kuongeza thamani ya mifugo kwa kunenepesha kabla ya kuchinja
- Kuzalisha kwa mikataba
- Kuwekeza kwenye machinjio zenye ubora wa kimataifa na viwanda vya kuongeza thamani nyama na bidhaa zake

Fursa

- Kuwepo kwa soko la migodini, mahoteli ya kitalii na supermarket
- Mahitaji makubwa (takwimu) ya nyama ya tanzania katika nchi za uarabuni

Madhara

Kuendelea kuingiza nyama kutoka nchi jirani

Changamoto

- Kuwa na kumbukumbu/takwimu sahihi za uzalishaji, biashara, usindikaji, uingizaji na uuzaji nje wa mifugo, nyama na bidhaa zake
- Kuzalisha nyama yenye kukidhi mahitaji ya soko ya ubora, kiasi na kupatikana kwa wakati
- Kufanyakazi kwa machinjio na kutumia kiasi kikubwa cha uwezo wa machinjio zilizopo
- Kutii sheria zinazoongoza tasnia ya nyama bila shuruti